



**DENVER
HEALTH**
— est. 1860 —
FOR LIFE'S JOURNEY

Ili kujilinda mwenyewe, familia
yako na jamii yako...

PATA CHANJO DHIDI YA COVID-19



Kwa nini upate chanjo?

Chanjo ni zana tunayotumia kukabiliana na COVID-19. Unawalinda wengine na unaisaidia JAMII yako.

Je, chanjo ni salama?

NDIYO Chanjo za COVID-19 zina ufanisi wa juu katika kukuinga dhidi ya COVID-19. Chanjo hizi haziwezi kukuambukiza ugonjwa.




Je, inatolewa bila malipo?

Ndiyo! Dozi zote za chanjo ni za BILA MALIPO kwa KILA MTU - bila kujali umri, mbari, kabila, hali ya makazi au uandikishaji nchini. Aina yoyote ya picha inakubaliwa na iwapo huna kitambulisho kilicho na picha, watoa chanjo watashirikiana nawe ili kuhakikisha umepata chanjo.



Nitahisi vipi baada ya chanjo?

Baada ya kupata chanjo yako ya COVID-19, unaweza kupata baadhi ya athari. Hizi ni ishara za kawaida kwamba mwili wako unajenga kinga na huwa zinaisha baada ya siku chache.



Bado nitahitajika kuvaa barakoa?

NDIYO! Bado untahitajika kuvaa barakoa na kuweka umbali wa kimwili baada ya kupata kila dozi ya chanjo.

Naweza kupata vipi maelezo zaidi kuhusu chanjo?

Kwa taarifa mpya zaidi.

1. Piga Simu ya Usajili wa Chanjo ya COVID katika **303-436-7000** na ubonyeze 3 kwa usaidizi katika lugha unayopendelea.
2. Fungua kamera ya simu yako na uchanganue msimbo wa QR; au
3. Tembelea **DenverHealth.org/covidvaccine**.

